# 1. Utangulizi

Toleo hili la Darubini ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 linaelezea utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025 katika mikoa ya kanda ya Kaskazini. Mikoa hiyo ni Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Tanga. Toleo hili litaonesha ni kwa kiasi gani Serikali imetekeleza nguzo zote za Dira 2025 katika Kanda hii. Nguzo hizo ni: (i) Kuboresha hali ya maisha ya Watanzania; (ii) Kuwepo kwa mazingira ya amani,utulivu na umoja; (iii) Kujenga utawala bora na utawala wa sheria; na (iv) Kujenga uchumi imara unaoweza kuhimili na ushindani kutoka nchi nyingine.

# 2. Utekelezajiwanguzoza Dira 2025

Pamoja na kuelezea hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali kutekeleza nguzo za Dira 2025 katika Kanda ya Kaskazini, sehemu hii inaelezea mafanikio yaliyopatikana na changamoto zilizopo.


## *2.1 Utekelezaji wa nguzo ya kwanza ya Dira 2025: Kuboresha hali ya maisha ya Watanzania*

Nguzo ya kwanza ya Dira 2025 iliweka malengo yafuatayo: Kuwa ifikapo mwaka 2025 Tanzania: (i) iwe na usalama wa chakula; (ii) itoe elimu ya msingi kwa watoto wote; (iii) uwepo usawa wa kijinsia kwenye masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa; (iv) iwe na huduma bora za afya kwa wananchi wote; (v) itoe huduma bora za afya ya uzazi kwa rika mbalimbali; (vi) ipunguze vifo vya watoto wachanga na vifo vya wanawake vitokanavyo na uzazi; (vii) kuwepo na maji safi na salama; (viii) wastani wa umri wa kuishi uongezeke kufikia kiwango cha nchi za kipato cha kati; na (ix) iondokane na umaskini uliokithiri. Sehemu hii itaeleza jinsi gani Serikali imetekeleza malengo hayo katika Kanda ya Kaskazinina changamoto zilizopo.

Katika kuhakikisha uwepo wa usalama wa chakula, Serikali ya Tanzania imekuwa ikigharamia miradi mbalimbali ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji nchini ili kukuza uzalishaji katika sekta ya kilimo na kuwawezesha wananchi wote kumudu bei za chakula. Miradi hiyo inatekelezwa kupitia Programu ya Kukuza Maendeleo katika Sekta ya Kilimo nchini (ASDP[1]), Mpango Kabambe wa Umwagiliaji Maji Mashambani (NIMP[2]), Mpango wa kuendeleza kilimo cha umwagiliaji katika mabonde ya Pangani na Rufiji, Mipango ya Maendeleo ya Kilimo Wilaya (DADPs[3]),Programu Husishi ya Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani (PIDP[4]) na miradi mingine ya maendeleo ya kilimo kwa kushirikiana na wafadhili wa nchi zilizoendelea. Baadhi ya skimu na mabwawa ya umwagiliaji yaliyojengwa na kukarabatiwa chini ya programu hizo katika mikoa iliyopo Kanda ya Kaskazini kuanzia mwaka 2000 hadi 2013 yameainishwa katika jedwali lifuatalo:

| Mkoa | Mabwawa ya umwagiliaji | Skimu zilizojengwa/kukarabatiwa |
|---|---|---|
| Arusha | Kiserian (hekta 30) | Ngage - Simanjiro (hekta 650); Mang'ola Prison Farm - Karatu (hekta 450), Mbuguni Shango - Arumeru (hekta 650); na pia familia 235 zimenufaika na skimu ya Lekitatu - Arumeru (hekta 464). |
| Tanga | Mkomazi - Korogwe (hekta 200); Misozwe-Muheza (hekta 100); Mwele-Muheza (hekta 100) | Misozwe - Muheza (hekta 100); Magoma - Korogwe (hekta 200); Kitivo - Lushoto (hekta 450); na pia zaidi ya familia 1600 zimenufaika na skimu za Mombo - Korogwe (hekta 220), Makorora - Korogwe (hekta 250); Kambi ya Tanga (hekta 410); Mahenge - Korogwe (hekta 300) na skimu ya Lemkuna (hekta 430). |
| Kilimanjaro | | Musa - Mwinjanga - Hai (hekta 676); Uraroni - Rombo (hekta 1,250); Mungushi na Kware - Hai; Kimwangamao - Moshi Vijijini (hekta 1,200); Nganjoni-Moshi Vijijini (hekta 220); Lawate Kisangara - Hai (hekta 250); Lower Moshi (hekta 2300); Ghona (hekta 450); Kirya (hekta 350); Kikafu Chini (hekta 641); Siha - Hai (hekta 120) na pia zaidi ya familia 1700 zimenufaika na skimu za Kivulini - Mwanga (hekta 410); Long'oi - Hai (hekta 300) na Soko - Moshi (hekta 370). |
| Manyara | | Babati; Dongobesh - Mbulu (hekta 200); Guwang - Mbulu (hekta 110); Gehandu; Dirma; Gichameda - Babati (hekta 154); Qash - Babati (hekta 206); Diyomat - Mbulu (hekta373); Harsha - Mbulu (hekta 250);Tumati - Mbulu, (hekta 112); Mangisa - Mbulu (hekta 190). |


Vilevile, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Ushirika imekuwa ikitoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kilimo Wilaya ambapo kwa mwaka 2003, mikoa ya kanda ya Kaskazini ilipokea zaidi ya milioni shilingi 800 ili kutekeleza miradi katika vijiji 22 (Arusha), vijiji 32 (Kilimanjaro), vijiji 34 (Manyara) na vijiji 14 (Tanga). Kutokana na jitihada hizo, kumekuwa na ongezeko la uzalishaji wa mazao ya chakula kama vile mahidi katika mikoa ya Kanda ya Kaskazini kama inavyooneshwa katika mchoro ufuatao.





Katika mikoa ya Tanga na Manyara, uzalishaji ulipungua kwa mwaka 2010 kutokana na hali ya ukame iliyotokana na mvua za vuli kunyesha chini ya kiwango cha kawaida na mvua za masika kuchelewa kuanza kunyesha. Hali hii pia iliathiri uzalishaji wa kitaifa kwa ujumla ambapo palikuwa na upungufu wa nafaka wa takriban tani milioni 1.3 uliotokana na uzalishaji mdogo wa mazao hayo wa tani milioni 5.2, ikilinganishwa na mahitaji ya nafaka ya jumla ya tani milioni 6.5. Aidha, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na kwa kushirikiana na uongozi wa mikoa ya Kanda ya Kaskazini wanaendelea kutoa mafunzo kwa wagani, wakulima na wadau mbalimbali kuzingatia kanuni za kudhibiti magonjwa yanayoshambulia mazao shambani ili mavuno yawe ya kutosha. Hadi kufikia mwaka 2013, washiriki takribani 1,500 kutoka Kanda ya Kaskazini walipata mafunzo hayo. Hata hivyo, juhudi zaidi zinahitajika katika kukuza kilimo cha umwagiliaji ili mazao yaweze kustawi vizuri.

Kulingana na takwimu za mwaka 2012, mkoani Arusha, eneo linalofaa kwa umwagiliaji ni hekta 45,397 na lililoendelezwa ni hekta 23,210 tu, sawa na asilimia 51ya eneo lote la umwagiliaji. Mkoani Kilimanjaro, eneo linalofaa kwa umwagiliaji ni hekta 579,700 na lililoendelezwa hekta 53,875 tu, sawa na asilimia 9 tu ya eneo lote linalofaa kutumika kwa umwagiliaji, Mkoa wa Manyara eneo linalofaa kwa umwagiliaji ni hekta 35,086 zinazotumika ni hekta 11,715 tu, sawa na asilimia 33 ya eneo lote la umwagiliaji. Takwimu hizi zinaonyesha bado kuna fursa kubwa sana katika kilimo cha umwagiliaji kwenye mikoa hii.Pamoja na mafanikio haya, kumekuwepo na changamoto nyingi katika kutekeleza nguzo hii. Kati ya hizo changamoto kubwa ni wakulima wengi kukosa elimu ya kutosha juu ya kilimo cha kisasa, kukosekana kwa soko la mazao ya wakulima na upatikanaji wa pembejeo kwa bei nafuu na kwa wakati.

Katika kutekeleza Dira 2025, Serikali imeendelea kuhakikisha elimu ya msingi inatolewa kwa watoto wote, ambapo mwaka 2000, Serikali iliondoa ada katika shule za msingi za Serikali. Pia jitihada mbalimbali zimefanyika katika kurahisisha upatikanaji wa elimu, kwa kujenga shule nyingi zaidi kama takwimu za Wizara ya Elimu zinavyoonesha kwenye mchoro ufuatao:




Ongezeko la idadi ya shule limeenda sambamba na ongezeko la asilimia ya watoto wenye umri kati ya miaka 7 hadi 13 wanaosoma katika shule za msingi. Ongezeko hilo limeonekana katika mikoa yote ya Kanda ya Kaskazini, isipokuwa katika mkoa wa Manyara, kama tawimu zinavyoonesha:





| | Tanga | Kilimanjaro | Manyara | Arusha |
|---|---|---|---|---|
| Mwaka 2013 | 99.3 | 90.2 | 79.8 | 92.8 |
| Mwaka 2003 | 92.9 | 90.1 | 83.6 | 87.5 |

Changamoto kuu katika nguzo hii ya utowaji wa elimu ya msingi kwa wote ni kushuka kwa kiwango cha elimu. Hali hii imesababishwa na upungufu wa walimu wenye sifa zinazotakiwa, vitabu vya kujifunzia na kiada vyumba vya madarasa na nyumba za walimu. Changamoto nyingine ni tatizo la wanafunzi wanaoandikishwa darasa la kwanza kutohitimu darasa la saba. Mfano katika mkoa wa Manyara, kati ya wanafunzi 40,616 walioanza darasa la kwanza mwaka 2006 ambao wamehitimu darasa la Saba mwaka 2013, jumla ya wanafunzi 10,628, sawa na asilimia 26 waliacha shule kutokana na sababu mbalimbali, zikiwemo utoro na mimba.

Serikali imeendelea pia kutilia mkazo suala la usawa wa kijinsia, kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Katika kutekeleza hilo, Wizara ilianzisha Dawati la Jinsia (Gender Desk) katika kila Wizara, Idara zinazojitegemea, Mikoa na Halmashauri ili kuhakikisha kuwa masuala ya jinsia yanazingatiwa na usawa unapatikana. Pia, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali huratibu maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani tarehe 08 Machi, kila mwaka. Lengo la maadhimisho haya ni kuwakutanisha wanawake ili waweze kubadilishana uzoefu katika kuzitafutia ufumbuzi changamoto mbalimbali zinazowakabili. Katika Kanda ya Kaskazini, maadhimisho ya kitaifa yalifanyika mkoani Arusha mwaka 2012.

Ili kuboresha upatikanaji wa huduma bora za afya kwa wananchi wote, taarifa za Ofisi ya Takwimu ya Taifa zinaonyesha kuwa Serikali imeongeza ujenzi wa hospitali, zahanati na vituo vya afya katika mikoa iliyopo katika Kanda ya Kaskazini kama inavyoonesha kwenye mchoro ufuatao:




Ongezeko hili la vituo ya kutolea huduma za afya limechangia kupunguza vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano katika kanda ya Kaskazini kutoka wastani wa vifo 98 kati ya watoto 1,000 wanaozaliwa wakiwa hai mwaka 2002, hadi kufikia wastani wa vifo 58 kati ya watoto 1,000 waliozaliwa wakiwa hai katika mwaka 2010. Changamoto iliyopo ni suala la vifaa vya hospitali havitoshelezi mahitaji. Kwa mfano katika baadhi ya hospitali za Serikali wagonjwa wanaolazwa ni wengi kuliko idadi ya vitanda vilivyopo. Hivyo, kupelekea baadhi ya vitanda kutumiwa na zaidi ya mgonjwa mmoja na wagonjwa wengine hulala chini.

Katika kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama,Serikali imeanzisha na kuendeleza miradi ya maji ya kitaifa. Katika Kanda ya Kaskazini, mradi mkubwa wa kitaifa, ni mradi wa Maji wa Handeni katika Wilaya ya Korogwe, ambao una vituo vya pampu sita, matanki ya kuhifadhi maji 56, vituo vya kuchotea maji 163, na waliunganisha mitandao ya maji 703. Mradi huo unahudumia vijiji 79 namji wa Handeni, wenye zaidi ya watu 80,000. Miradi mingine ya maji safi iliyoanzishwa mkoani Tanga ni Irente (Lushoto); Kwamndolwana Kwameta (Korogwe); Ubembe, Nkumba,Kwemhozi (Korogwe); Bumbuli, Kweminyasa (Bumbuli); Madanga na Bweni (Pangani); Misima, Suwa Kwkoma, Suwa Kwimba (Handeni); Kikunde na Negero (Kilindi); na Daluni-Kibaoni (Mkinga). Miradi hii imewezesha vijiji 21 vyenye wakazi 44,557 kupata majisafi na salama karibu na makazi yao.

Mkoani Arusha, miradi ya maji chini ya mpango wa kulenga Matokeo Makubwa Sasa (BRN) inatekelezwa katika vijiji mbalimbali,vikiwemo Patanumbe, Kikuletwa, Ugoro, Valeska, Majengo, Mbuguni, Moivaro, Ndoombo, Nshupuna King'oro, ambapo zaidi ya wananchi 100,000 wananufaika. Miradi hii ilianzishwa mwaka 2013.

Mkoani Manyara, Serikali pia imeendelea kuboresha upatikanaji wa maji safi na salama kupitia ujenzi na ukamilishaji wa miundombinu ya maji katika vijiji mbalimbali kwa kila halmashauri kama ifuatavyo: Babati (Endagile, Gedamar, Managhana, Riroda, Mutuka, Darakuta-Minjingu, Luxmanda/Secheda, Tsamasi,Seloto, Erri, Bashnet-Saria, Ufana, Chemchem, Himiti, Kiongozi, Malangi, Managhat, Nakwa, Harra, Hallanalmbilili); Mbulu (Masieda, Dongobesh, Maretaduchini, Endamasak, Tumati, Mongahay, Harsha, Singu, Moringa, Endanyawish na Eshkesh); Hanang (Getasam, Ng'alda, Gidagarbu,Ishponga, Simbay, Galangal, Garawja, Masakta, Endasiwold, Endasak, Endagaw); Kiteto (Mwanya, Ndorkkon, Njiapanda, Eseki, Dosidosi, Kona naLoolera); Simanjiro (Loswaki, Lorokare, Gunge, Loibosiret, Olchoronyori, Naisinyai na Olbili).

Serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali ili kuondoa umaskini uliokithiri kwa wananchi hasa walio vijijini. Jitihada hizo ni pamoja na Mpango wa kunusuru kaya maskini unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii, TASAF. Takwimu za TASAF zinaonesha kuwa hadi kufikia mwaka 2012, jumla ya

1 Agricultural Sector Development Programme
2 National Irrigation Master Plan
3 District Agricultural Development Programmes
4 Participatory Irrigation Development Programme

miradi ya maendeleo 1,641imeanzishwa katika mikoa iliyopo Kanda ya Kaskazini kupitia mfuko huo na zaidi ya wananchi 1,800,000 wamenufaika.

### 2.2 Utekelezaji wa nguzo ya pili ya Dira 2025 - Kuwepo kwa mazingira ya amani, utulivu na umoja

Nguzo ya pili ya Dira 2025 inalenga kuimarisha amani, utulivu na umoja wa nchi,ili kustawisha maendeleo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Sehemu hii itaeleza jinsi gani Serikali imetekeleza malengo hayo katika Kanda ya Kaskazinina changamoto zilizopo.

Pamoja na kwamba ni jukumu la kila Mtanzania na kila raia mwema kushiriki kikamilifu kulinda amani na utulivu wa nchi, Serikali imekuwa ikiongoza jitihada hizo kupitiaJeshi la Polisi, ambalo limekuwa likiendeshaoperesheni mbalimbali kukamata wahalifu na kuwafikisha mahakamani.Katika mikoa iliyopo Kanda ya Kaskazini, Jeshi la Polisi lilifanikiwa kuwakamata zaidi ya wahamiaji haramu 600 mwaka 2007 na kuwafikisha mahakamani. Idadi hiyo iliongezeka hadi kufikia wahamiaji haramu zaidi ya 700 katika mwaka 2012. Pia,utekelezaji wa Mpango wa Ulinzi Shirikishi ulioanzishwa na Jeshi la Polisi mnamo mwaka2007 umesaidia kupunguza hali ya uhalifu katika mikoa ya Kanda ya Kaskazini, ambapo katika mkoa wa Manyara uhalifu umepungua kwa zaidi ya asilimia 85 hadi kufikia mwaka 2012. Pia, takwimu za matukio ya uhalifu mkoa wa Kilimanjaro zimepungua kutoka 32,078 mwaka 2011 ikilinganishwa na matukio 29,008 mwaka 2012.Vilevile, katika mkoa wa Tanga, takwimu za Jesji la Polisi zinaonesha kupungua kwa makosa ya jinai kutoka makosa 17,297 mwaka 2006, hadi kufikia makosa 17, 747, sawa na upungufu wa asilimia 2.5. Hii imetokana na juhudi zaidi zinazofanywa na Jeshi la Polisi, kwa kushirikiana na wananchi katika kuimarisha usalama wa nchi kupitia misako maalum pamoja na utekelezaji wa ulinzi shirikishi.

Kuhusu wahamiaji haramu na biashara haramu, Jeshi la Polisi limekuwa likipambana kuwabaini na kuwakamata wahamiaji haramu hususan kutoka nchi za Somalia na Ethiopia. Mikoa iliyopo Kanda ya Kaskazini ambayo imekuwa ikiongoza kwa kuwa na wahamiaji haramu wengi ni Kilimanjaro ambapo wahamiaji haramu 488 walikamatwa na Tanga ambapo wahamiaji haramu 31 walikamatwa mwaka 2012.

Pamoja na mafanikio hayo, katika kanda ya Kaskazini hasa mkoani Arusha kumekuwa na matukio yanayoashiria uvunjifu wa amani kama mabomu, kumwagiwa tindikali, viongozi wa dini kuuawa, maandamano ya vurugu, ukabila, ubaguzi wa rangi na udini.

### 2.3 Utekelezaji wa nguzo ya tatu ya Dira 2025 - Kujenga utawala bora

Nguzo ya tatu ya Dira 2025 imelenga kuimarisha utawala bora na utawala wa sheria kwa kujenga jamii yenye sifa zifuatazo (i) maadili mema na kuthamini utamaduni; (ii) uadilifu na kuheshimu utawala wa sheria; (iii) isiyokuwa na rushwa na maovu mengine; na (iv) iliyoelimika na inayojiamini, inayojifunza kutokana na uzoefu wake na wa wengine, na yenye kumiliki na kubaini ajenda za maendeleo.

Ili kujenga uadilifu na kuheshimu utawala wa sheria, mnamo mwaka 2007, Serikali ilianzisha Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), ili kuondoa athari za rushwa katika maendeleo ya jamii kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni. Taasisi hiyo imekuwa ikifanya tafiti mbalimbali ili kubaini mianya ya rushwa na kuweka mikakati ya kuitokomeza. Katika mkoa wa Manyara uliopo Kanda ya Kaskazini, TAKUKURU,kwa kushirikiana na viongozi wa Halmashauri ya Mji na Halmashauri za Wilaya,iliweka mikakati wa kudhibiti mianya ya rushwa na matatizo yaliyojitokeza katika ugawaji wa vocha za pembejeo za kilimo mwaka 2008. Pia katika mkoa wa Tanga, TAKUKURU imedhibiti mianya ya rushwa katika Shirika la Nyumba tawi la Tanga, ambapo mojawapo ya mikakati iliyofanikisha jambo hilo ni uhakiki wa wateja ili kujua idadi ya wapangaji wake halali na wale waliobainika sio halali,kufuata hatua sahihi za kupeleka maombi. Mkoani Arusha, mwaka 2010 TAKUKURU iliweza kudhibiti rushwa na matumizi mabaya ya fedha za ruzuku kwa ajili ya miradi ya maendeleo kupitia utafiti uliofanyika katika Halmashauri ya manispaa ya Arusha na ya wilaya ya Monduli.

Ili kujenga jamii iliyoelimika, Serikali mnamo mwaka 2009 kupitia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, iliweka kipaumbele kwa wanafunzi wa masomo ya sayansi na ualimu, kwa kuwapatia asilimia 100 ya fedha za mkopo. Lengo ni kuhamasisha wanafunzi wengi kusoma masomo ya sayansi na ualimu, ili kuziba pengo lililopo la wataalamu katika taaluma hizo. Pia, Serikali kupitia wizara ya Kilimo imekuwa ikiandaa maonesho ya Nanenane kila mwaka ili kutoa elimu kwa wakulima na kufanya kilimo kiwe na tija zaidi. Katika mwaka 2013, kilele cha maonesho ya Nanenane kilikuwa katika kanda ya Kaskazini ambapo kauli mbiu ilikuwa "Zalisha Mazao ya Kilimo na Mifugo kwa Kulenga Mahitaji ya Soko". Zaidi ya hayo, jamii ya imeonesha ari ya kuelimika na kujifunza kwa kushiriki semina mbalimbali zinazoandaliwana Serikali. Mfano mmojawapo ni ushiriki wa wananchi katika semina zinazohusu umuhimu wa chanjo kwa watoto ambapo takwimu za Wizara ya Afya zinaonesha kuwa hadi kufikia mwaka 2010, asilimia 80 ya watoto walio na umri kati ya miezi 12 hadi 23 walipata chanjo zote, kutokana na mwamko na uelewa wa wazazi juu ya umuhimu wa chanjo hizo.

Jitihada nyingine za kujenga jamii iliyoelimika na inayojiamini ni uanzishwaji wa maadhimisho ya Wiki ya Elimu nchini mwaka 2014,chini ya Wizara ya Elimu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI. Lengo la maadhimisho hayo ni kuelimisha umma juu ya umuhimu wa kila mwananchi kuchangia katika kuchochea ari ya kuwa na elimu bora. Jedwali lifuatalo linaonesha idadi ya shule zilizopata tuzo kwa ufaulu mzuri katika kanda ya Kaskazini:

| Mkoa | Shule za Msingi | Shule za Sekondari | Jumla |
|---|---|---|---|
| Arusha | 130 | 23 | 153 |
| Kilimanjaro | 194 | 32 | 226 |
| Manyara | 145 | 1 | 146 |
| Tanga | 376 | 11 | 387 |

### 2.4 Utekelezaji wa nguzo ya nne ya Dira 2025: Kujenga uchumi imara unaowezakuhimili ushindani

Nguzo ya nne ya Dira 2025 imelenga kujenga uchumi imara unaoweza kuhimili ushindani kutoka nchi nyingine. Lengo hilo limepangwa kutimizwa kwa kujenga sekta shindani ya Viwanda, Biashara, Masoko na Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo ili kujenga uchumi endelevu na kufikia maendeleo ya viwanda kwa kiwango cha kati ifikapo mwaka 2025.

Wizara mojawapo inayohusika katika kutekeleza nguzo ya nne ya Dira 2025 ni Wizara ya Ujenzi kupitia miradi ya ujenzi wa barabara ili kufungua fursa za maendeleo katika maeneo mbalimbali ya nchi, kwani barabara nzuri hurahisisha upatikanaji wa bidhaa na huduma. Katika mikoa iliyopo Kanda ya Kaskazini, Serikali imefanikisha ujenzi wa barabara zifuatazo kwa kiwango cha lami:

| Mkoa | Barabara | Urefu wa barabara (kilometa) | Mwaka wa ujenzi hadi kukamilika |
|---|---|---|---|
| Arusha | Arusha - Holili | 140 km | 2014 - (Unaendelea) |
| | Bonga - Babati | 19.2km | 2010 - 2012 |
| | Arusha - Namanga | 105 km | 2008 - 2013 |
| | Makutano - Natta - Mugumu | 80 km | 2013 - (Unaendelea) |
| Kilimanjaro | Marangu - Rombo Mkuu | 32 km | 2008 - 2013 |
| | Rombo Mkuu - Tarakea | 32km | 2006 - 2012 |
| | Mwika - Kilacha | 32km | 2008 - 2013 |
| | Sanya Juu (Siha) - Kamwanga | 75km | 2013 - (Unaendelea) |
| Tanga | Korogwe - Handeni | 65km | 2009 - 2013 |
| | Handeni - Mkata | 54km | 2009 - 2013 |
| | Tanga - Horohoro | 65km | 2009 - 2012 |
| | PMMR Tanga East | 116.8 km | 2009 - 2013 |
| | PMMR Tanga West | 224.8 km | 2009 - 2014 |
| Manyara | Katesh - Dareda | 73.8 km | 2008 - 2011 |
| | Dareda - Minjingo | 84.6 km | 2008 - 2012 |

Serikali pia imefanya jitihada ya kuongeza viwanda kwa ajili ya kuongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa Tanzania na kuuzwa nje ya nchi. Jitihada hizo ni pamoja na uanzishwaji Mamlaka ya Kusimamia Maeneo Huru ya Uzalishaji (EPZA[5])mnamo mwaka 2006 ambapo ndani ya maeneo hayo miundombinu iliyoboreshwa na vivutio hutolewa kwa wawekezaji, lengo likiwa ni kukuza uwekezaji ambao utalenga kuimarisha uuzaji bidhaa nje ya nchi na kuongeza mapato ya nchi. Katika Kanda ya Kaskazini, eneo huru la uwekezaji lilizinduliwa rasmi mkoani Tanga mwaka 2013 katika eneo la Pongwe, na mwaka 2015 eneo lenye hekta 1,363limetengwa katika eneo la Neema, Tanga. Maandalizi ya kuanzisha maeneo huru ya uwekezaji katika mikoa ya Kilimanjaro na Manyara (Mirerani) bado yanaendelea.

Serikali imebuni imebuni pia mikakati kadhaa ya kuboresha Sekta ya Mifugo katika Kanda ya Kaskazini, hususani kunenepesha mifugo kwa muda mfupi na kuiuza kwa nzuri zaidi, kuboresha magulio ya mifugo na mazao yake, kuhamasishaji uwekezaji wa viwanda vya mazao mbalimbali ya mifugo kama vile ngozi na maziwa ili kuongeza thamani ya mazao ya mifugo. Katika kanda ya Kaskazini, Serikali ilitoa vibali kwa wawekezaji wa ndani kuanzisha viwanda kama Viwanda vya usindikaji nyama Simanjiro na Arusha, Viwanda vya usindikaji wa maziwa katika wilaya za Arusha, Tanga, Karatu, Babati, Simanjiro, Hai na Moshi vijijini na usindikaji wa ngozi kupitia vikundi vidogo vidogo chini ya Kampuni mbalimbali, kama vile Asilia Ltd.

**Economic and Social Research Foundation (ESRF)**
P.O. Box 31226, Dar es Salaam, Tanzania.
Phone: (+255) 754 780 133, (+255) 777 790 133,
(+255) 782 780 133 • Fax: (+255 22) 2760062
E-mail: esrf@esrf.or.tz • Website: www.esrf.or.tz

[5] *Export Processing Zones Authority*

# DARUBINI YA DIRA YA MAENDELEO YA TAIFA 2025

## Toleo la Kanda ya Kaskazini



Toleo la TANO

ESRF